



# NEWS RELEASE

## **MAONESHU YA 47 YA BIAHARA YA KIMATAIFA YA DAR ES SALAAM TAREHE 28 JUNI HADI 13 JULAI, 2023**

Uongozi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) unayo furaha kuwakaribisha Waoneshaji wa bidhaa na Watembeleaji katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoanza leo tarehe **28 Juni hadi 13 Julai, 2023** katika Uwanja wa Maonesho wa Mwl J.K. Nyerere, Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam.

1. Maonesho haya yatafunguliwa kila siku kuanzia **saa 4.00** asubuhi hadi **saa 12.00 jioni**
2. Aidha Waoneshaji wanaombwa kufuata Taratibu, Sheria na Kanuni zinazotakiwa katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam
3. Kwa mara nyingine tena, mwaka huu, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) kwa mara ya kwanza imeandaa Banda Maalum la Expo Village, programu maalumu ya kilimo, madini, teknolojia ya Habari, siku ya nchi mbalimbali na utaratibu kwa watembeleaji wa kutumia huduma ya VIP wakati wa Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam

Washiriki wanaotumia mabanda ya waoneshaji wengi kama vile Banda la Karume, Banda la SabaSaba, Jakaya Mrisho Kikwete, Benjamini Mkapu Ali Hassan Mwinyi, na eneo la Mahema ya Manyara na Mikumi wanashauriwa kufika kwenye mabanda yao saa **2.30 asubuhi ili kusubiri muda wa kufungua mabanda ambao ni saa 4.00 asubuhi. Endapo mshiriki/washiriki hawatakuwepo wakati Mabanda hayo yakifunguliwa kwa muda uliotajwa hapo juu, TanTrade haitahusika na upotevu wa aina yoyote.**

4. Waoneshaji wote wanahimizwa kuziwekea bima bidhaa zao. Aidha waoneshaji wanashauriwa kuwasilianana na watoa huduma ya bima waliopo katika Uwanja huu wa Maonesho au watoa bima wengine. TanTrade haitahusika na upotevu utakaotokea.
5. Uvutaji wa **SIGARA** kwenye Kumbi za Maonesho ni **Marufuku wakati wote**.
6. Washiriki wote wanakumbushwa na kusesitizwa kuwa **HAIRUHUSIWI KUPIGA MUZIKA AU NGOMA ZA UTAMADUNI KATIKA MAONESHU WAKATI WOTE**. Ukiukaji wa agizo hili utasababisha mhusika kunyang'anywa vifaa vyake ili kuepuka usumbufu kwa wenzake.
7. Hakikisha ulinzi wa bidhaa zako na mali wakati wote wa Maonesho ili kuepuka udokozi unaoweza kujitokeza. Endapo kuna udokozi umejitokeza, toa taarifa katika Kituo cha Polisi kilichopo nje kwenye Lango Kuu la kuingilia uwanjani.
8. Ni marufuku kwa mshiriki yeyote kutumia eneo zaidi ya lile aliloruhusiwa kama vile "korido" na barabara kwa kuuzia au kuonesha bidhaa zake, atakayevunja sharti hili bidhaa zake zitazuiliwa.
9. Mauzo yatafanyika katika sehemu zilizoruhusiwa tu na mauzo yote yanahitajika kuwa na Ushuru wa Stampu na kulipiwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa mujibu wa Sheria. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambao wana ofisi ndani ya **Kurugenzi ya DTM ya TanTrade idara ya Taarifa za biashara** watakuwa tayari kutoa ushirikiano wao ili kufanikisha jambo hili.
10. Kwa taarifa zaidi, tafadhali usisite kuwasiliana na Kurugenzi ya Ukuzaji Biashara iliyopo karibu na mlango wa kuingilia uwanjani.

**UTAWALA**